TANGAZO LA SERIKALI Na. 149 la tarehe 7/3/2025

SHERIA YA CHUO CHA ELIMU YA BIASHARA
(SURA YA 315)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 14(1))*

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA NIDHAMU KWA WANAFUNZI ZA MWAKA 2025

Jina
TS Na. 365 la 2024

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Nidhamu kwa Wanafunzi za Mwaka 2025 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Nidhamu kwa Wanafunzi za Mwaka 2024, ambazo katika Kanuni hizi zinarejewa kama "Kanuni kuu".

Kufuta na kuandika upya kanuni ya 4

**2**. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta na kuandika upya kanuni ya 4 kama ifuatavyo:

Makosa ya kinidhamu

**4**. Kwa madhumuni ya Kanuni hizi, makosa ya kinidhamu yatajumuisha-

(a) mwenendo ambao unafanya au unaweza kusababisha uharibifu au vurugu kwa mtu au mali yoyote ndani ya Chuo, endapo kitendo hicho kimefanywa na mwanafunzi dhidi ya mwanafunzi mwingine au afisa, chuoni au eneo lolote lililokodishwa au linalotambuliwa rasmi na Chuo;

(b) kitendo au mwenendo ambao unaweza kuzuia au kukwamisha kufanyika kwa shughuli yoyote ya

kitaaluma, kiutawala au uchaguzi Chuoni;

(c) kumiliki mali yoyote ya Chuo bila kibali;

(d) kukataa au kushindwa kutii amri halali au maelekezo yaliyotolewa na afisa yeyote wa Chuo au amri iliyotolewa na chombo chochote cha Chuo chenye mamlaka;

(e) kwa makusudi na kwa kujua, kutoa taarifa ya uongo kwa afisa yeyote wa Chuo;

(f) kushindwa au kukataa bila sababu ya msingi kuhudhuria kikao kilichoitishwa na afisa, au chombo chenye mamlaka;

(g) kuzuia au kuingilia kwa makusudi majukumu au shauri lililoendeshwa na afisa au chombo chenye mamlaka;

(h) kukataa au kushindwa kutoa ushahidi bila sababu ya msingi mbele ya Kamati ya Nidhamu ya Wanafunzi au chombo kingine chenye mamlaka;

(i) kukataa au kushindwa kutekeleza hukumu, uamuzi au adhabu halali iliyotolewa na afisa yeyote wa Chuo au chombo cha Chuo chenye mamlaka;

(j) kutumia lugha ya kashfa, matusi au ya kitisho dhidi ya mwanafunzi mwingine, afisa au mwanajumuiya yeyote wa Chuo;

(k) kufanya kitendo chochote ambacho kinasababisha au

kinaweza kusababisha madhara ya kimwili au kisaikolojia kwa mwanafunzi mwingine, afisa au mwanajumuiya yeyote wa Chuo;

(l) kupiga kelele, kusumbua au kuwahamasisha wanafunzi au watu wengine kupiga kelele au kufanya usumbufu wa aina yoyote katika eneo la Chuo au maeneo yaliyokodiwa na Chuo;

(m) kuandaa, kushiriki au kuitisha mkutano, Baraza la Wanafunzi au kikao chochote bila kibali cha chuo;

(n) kuchochea au kushiriki katika ghasia, mgomo au kususia masomo;

(o) kupanga au kushiriki katika maandamano yasiyo halali;

(p) kumwalika kiongozi wa serikali au wa kisiasa, mgeni rasmi, mshereheshaji, au mtu yeyote kutoka nje ya Chuo bila kibali kutoka kwa Mshauri wa Wanafunzi au afisa mwenye mamlaka;

(q) kusambaza matamko ya kashfa kwa mtu mwingine;

(r) uzembe au ubadhirifu wa fedha za Serikali ya Wanafunzi, chama, klabu, au kikundi cha wanafunzi kinachotambulika;

(s) kiongozi wa Serikali ya Wanafunzi kuingia mkataba na mtu yeyote kinyume na

Katiba ya Serikali ya Wanafunzi;

(t) kukusanya fedha kwa ulaghai au kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kutoka kwa mwanafunzi mwenzake au mtu mwingine;

(u) kughushi, kuwasilisha au kusambaza nyaraka za uongo;

(v) kitendo chochote kinachofanywa na mwanafunzi ndani au nje ya Chuo na kupelekea kuharibu taswira ya Chuo;

(w) kuendesha mkutano au kampeni ya uchaguzi nje ya muda uliopangwa;

(x) unyanyasaji wa kijinsia wa aina yoyote ikijumuisha-

(i) kushinikiza kufanya tendo la ngono au upendeleo;

(ii) kuuliza kuhusu maisha binafsi ya kingono, kushawishi kupewa ngono kwa ahadi ya kutoa zawadi;

(iii) kutoa maoni ya udhalilishaji kutokana na umbo la mtu, kung'ang'ania kuomba miadi;

(iv) kufanya utani wa kingono, kutoa maoni ya kingono, kutumia lugha ya matusi, kutoa ishara ya kingono;

(v) kusema uongo au kueneza uvumi

kuhusu maisha ya kingono ya mtu kwa madhumuni ya kuharibu sifa za mlengwa;

(vi) kugusana kimwili kwa kusudio la kingono bila ridhaa;

(vii) kusambaza ujumbe wa shambulizi la kingono kwa njia yoyote;

(viii) kufanya ngono ya kundi, kubaka, shambulio la aibu, kuwa uchi au kubaka kwa kundi; na

(ix) matumizi ya mamlaka au madaraka kumshawishi mtu mwingine kuingia katika mahusiano ya kingono au kumuadhibu mtu kutokana na kukataa kwake.

(y) kujifanya mtu mwingine;

(z) kitendo chochote cha mwanafunzi chenye lengo la kuonesha ushiriki au utii kwa chama cha siasa;

Sura ya 95

(aa) kosa ambalo linavunja Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya;

Sura ya 329

(bb) kosa ambalo linavunja Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa;

(cc) kuingilia pasipo uhalali mchakato wa uchaguzi wa Serikali ya Wanafunzi;
(dd) kuunda au kuanzisha chama, klabu au kikundi cha wanafunzi bila kibali kutoka kwa Mshauri wa Wanafunzi, afisa ustawi wa jamii au chombo chenye mamlaka;
(ee) kushindwa kuonesha au kukabidhi kitambulisho cha mwanafunzi inapotakiwa kufanya hivyo na afisa mwenye mamlaka; na
(ff) Mshauri wa Wanafunzi au afisa ustawi wa jamii kutopitisha mawasiliano yoyote rasmi kwa ajili ya kwenda nje ya Chuo, kwa mwanafunzi yeyote au kiongozi wa Serikali ya Wanafunzi.

Marekebisho ya kanuni ya 5

**3.** Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 5 kwa-
(a) kufuta aya ya (a); na
(b) kuzibadili aya za (b) mpaka (q) kuwa aya ya (a) mpaka (p).

Kufuta na kuandika upya kanuni ya 8

**4.** Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta na kuandika upya kanuni ya 8 kama ifuatavyo:

Uharibifu au upotevu wa mali ya Chuo

**"8.**-(1) Mwanafunzi aliyekuwepo katika eneo ambalo uharibifu au upotevu wa mali ya Chuo umetokea, atatakiwa kutoa taarifa kwa Mshauri wa Wanafunzi au afisa Ustawi wa Jamii kuhusu mtu au

mwanafunzi aliyeharibu au kupoteza mali hiyo.

(2) Endapo mwanafunzi atashindwa kutoa taarifa za mtu au mwanafunzi aliyeharibu au kupoteza mali ya Chuo kama ilivyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1), gharama za kukarabati au kubadili mali hiyo zitachangiwa na wanafunzi wote waliokuwepo wakati wa uharibifu au upotevu huo."

Marekebisho ya kanuni ya 23

**5.** Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 23 (3) kwa kuongeza maneno "bila sababu ya msingi" Katikati ya maneno "hayupo" na "na alipewa".

Marekebisho ya kanuni ya 30

**6.** Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 30 (3) kwa kuongeza maneno "bila sababu ya msingi" katikati ya maneno "siku saba za kazi" na "tangu kupokea uamuzi".

Marekebisho ya Jedwali

**7.** Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta na kuandika upya Jedwali la Pili kama ifuatavyo:

________

"JEDWALI LA PILI

________

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 33(1))*

ADHABU KWA MAKOSA YA KINIDHAMU

| KANUNI | KOSA LA KINIDHAMU | ADHABU |
|---|---|---|
| 4 (a) | Mwenendo ambao unafanya au una uwezekano wa kusababisha uharibifu au vurugu kwa mtu au mali yoyote ndani ya Chuo ikizingatiwa kuwa, kitendo hicho kimefanywa na mwanafunzi dhidi ya mwanafunzi mwingine au afisa, Chuoni au eneo lolote lililokodishwa au linalotambuliwa rasmi na Chuo. | Mwanafunzi atapewa onyo kali au kusimamishwa masomo kwa muda usiozidi mwaka mmoja na ataagizwa kulipa fidia kwa thamani ya mali iliyoharibika. |
| 4 (b) | kitendo au mwenendo ambao unaweza kuzuia au kukwamisha kufanyika kwa shughuli yoyote ya kitaaluma, kiutawala au uchaguzi. | Mwanafunzi atasimamishwa masomo kwa muda usiozidi mwaka mmoja wa masomo. |
| 4 (c) | Kumiliki mali yoyote ya Chuo bila kibali. | Kutoa onyo kali na kumwagiza mwanafunzi kurudisha mali hiyo ikiwa na hali nzuri. Iwapo mali iliyorudishwa haitakuwa na hali nzuri, mwanafunzi atatakiwa kutoa fidia kwa mali aliyoharibu. |
| 4(d) | kukataa au kushindwa kutii amri halali au maelekezo yaliyotolewa na afisa yeyote wa Chuo au amri kutoka kwa chombo chochote cha Chuo chenye Mamlaka. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha mwanafunzi masomo kwa muda usiozidi miezi sita. |
| 4 (e) | kwa makusudi na kwa kujua, kutoa taarifa ya uongo kwa afisa yeyote wa Chuo. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi mitatu. |
| 4 (f) | kushindwa au kukataa bila sababu ya msingi kuhudhuria kikao kilichoitishwa na afisa au chombo chenye mamlaka. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha mwanafunzi masomo kwa muda usiozidi miezi sita. |
| 4(g) | kuzuia au kuingilia kwa makusudi majukumu au shauri lililoendeshwa na afisa au chombo chenye mamlaka. | Kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa mwaka mmoja. |
| 4 (h) | kukataa au kushindwa kutoa ushahidi bila sababu ya msingi mbele ya Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi au chombo chenye mamlaka. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi mitatu. |

| KANUNI | KOSA LA KINIDHAMU | ADHABU |
|---|---|---|
| 4 (i) | kukataa au kushindwa kutekeleza hukumu, uamuzi au adhabu halali iliyotolewa na afisa yeyote au chombo chenye mamlaka. | Kumsimamisha mwanafunzi masomo kwa muda usiozidi mwaka mmoja au kumfukuza mwanafunzi. |
| 4 (j) | mwanafunzi kutumia lugha ya kashfa, matusi au ya kitisho dhidi ya mwanafunzi mwingine, afisa au mwanajumuiya yeyote wa Chuo. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi sita. |
| 4 (k) | kufanya kitendo chochote ambacho kinasababisha au kinaweza kusababisha madhara ya kimwili au kisaikolojia kwa mwanafunzi mwingine, afisa au mwanajumuiya yeyote wa Chuo. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi mwaka mmoja. |
| 4 (l) | kupiga kelele, kusumbua au kuwahamasisha wanafunzi au watu wengine kupiga kelele au kufanya usumbufu wa aina yoyote katika eneo la Chuo au maeneo yaliyokodiwa na Chuo. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiopungua miezi mitatu. |
| 4 (m) | kuandaa, kushiriki, kuitisha mkutano, Baraza la Wanafunzi au kikao bila kibali. | kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi sita. |
| 4 (n) | kuchochea au kushiriki katika ghasia, mgomo au kususia madarasa. | Kumsimamisha mwanafunzi masomo kwa muda usiozidi mwaka mmoja. |
| 4 (o) | kupanga na kushiriki katika maandamano yasiyo halali. | kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi mwaka mmoja. |
| 4 (p) | kumwalika kiongozi wa Serikali au wa kisiasa, mgeni rasmi, mshereheshaji, au mtu yeyote kutoka nje ya Chuo bila kibali kutoka kwa Mshauri wa Wanafunzi au afisa mwenye mamlaka. | kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiopungua miezi mitatu. |
| 4 (q) | kusambaza matamko ya kashfa kwa mtu mwingine. | kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiopungua miezi mitatu. |
| 4(r) | uzembe au ubadhirifu wa fedha za Serikali ya Wanafunzi, chama, klabu, au kikundi cha wanafunzi kinachotambulika. | kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa mwaka mmoja na atatakiwa kurejesha fedha zilizofanyiwa ubadhirifu. |
| 4 (s) | kiongozi wa Serikali ya Wanafunzi kuingia mkataba na mtu yeyote kinyume na Katiba ya Serikali ya Wanafunzi. | Kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi sita na atawajibika binafsi kwa deni au madai yatakayolimbikizwa chini ya mkataba huo. |

*Tangazo la Serikali Na.149 (Linaendelea.)*

| KANUNI | KOSA LA KINIDHAMU | ADHABU |
|---|---|---|
| 4 (t) | kukusanya fedha kwa ulaghai au kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kutoka kwa mwanafunzi mwenzake au mtu mwingine. | Kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa mwaka mmoja na atatakiwa kurejesha fedha alizokusanya kwa ulaghai au udanganyifu. |
| 4 (u) | kughushi, kuwasilisha au kusambaza nyaraka za uongo. | Kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiopungua miezi sita. |
| 4 (v) | kitendo chochote kinachofanywa na mwanafunzi ndani au nje ya Chuo na kupelekea kuharibu taswira ya Chuo. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiopungua miezi mitatu. |
| 4 (w) | Kuendesha mkutano au kampeni ya uchaguzi nje ya muda uliopangwa. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi sita. |
| 4 (x) | Unyanyasaji wa kijinsia wa aina yoyote | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiopungua miezi sita. |
| 4 (y) | Kujifanya mtu mwingine. | Kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiopungua mwaka mmoja au kumfukuza. |
| 4(z) | kitendo chochote cha mwanafunzi chenye lengo la kuonesha ushiriki au utii kwa chama cha siasa. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi sita. |
| 4 (aa) | Kosa ambalo linavunja Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. | Kumfukuza masomo mwanafunzi. |
| 4(bb) | Kosa ambalo linavunja Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. | Kumfukuza masomo mwanafunzi. |
| 4 (cc) | Kuingilia pasipo uhalali mchakato wa uchaguzi wa Serikali ya Wanafunzi. | Kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiopungua miezi sita. |
| 4 (dd) | kuunda au kuanzisha chama, klabu au kikundi cha wanafunzi bila kibali kutoka kwa Mshauri wa Wanafunzi, afisa ustawi wa jamii au chombo chenye mamlaka. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi mitatu. |
| 4 (ee) | kushindwa kuonesha au kukabidhi kitambulisho cha mwanafunzi inapotakiwa kufanya hivyo na afisa mwenye mamlaka. | kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi mitatu. |
| 4 (ff) | kutokupitisha kwa Mshauri wa Wanafunzi au afisa ustawi wa jamii mawasiliano yoyote rasmi ya kwenda nje ya Chuo kwa mwanafunzi yeyote au kiongozi wa Serikali ya Wanafunzi. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi mitatu. |

ADHABU KWA MAKOSA YA KINIDHAMU YANAYOHUSIANA NA UVAAJI WA MAVAZI WA WANAFUNZI

| KANUNI | KOSA LA NIDHAMU | ADHABU |
|---|---|---|
| 5(a) hadi (p) | Mwanafunzi yeyote atakayevunja Kanuni ya 5 (1) (a) hadi (p). | (a) Mwanafunzi atazuiwa kuingia kwenye majengo ya Chuo au majengo yoyote yaliyopangwa na Chuo;<br>(b) Mwanafunzi atazuiwa kuingia kwenye Ofisi za Chuo, kumbi za mihadhara au madarasa, maktaba, maabara na mikusanyiko yote rasmi; au<br>(c) Mwanafunzi atasimamishwa masomo kwa muda usiozidi miezi mitatu. |

ADHABU KWA MAKOSA YA KINIDHAMU YANAYOHUSIANA NA MALAZI

| KANUNI | KOSA LA NIDHAMU | ADHABU |
|---|---|---|
| 6 (a) | Kupangisha chumba katika mabweni ya Chuo au malazi mengine yaliyokodiwa au kutambuliwa na Chuo kwa mtu mwingine | Kumwondoa mwanafunzi bwenini bila kumrudishia malipo ya pango. |
| 6 (b) | Kuishi kwenye bweni la Chuo au malazi mengine yaliyokodiwa au kutambuliwa na Chuo pasipo uhalali. | Kulipa asilimia 30 ya malipo ya mwaka ya pango na kufukuzwa bwenini au malazi husika |
| 6 (c) | Kutumia majengo ya mabweni kwa ajili ya matukio ya kijamii bila kupata kibali cha Mshauri wa Wanafunzi au afisa ustawi wa jamii. | Kumwondoa mwanafunzi bwenini bila kumrejeshea malipo ya pango. |
| 6 (d) | Kuchangia chumba na mwanafunzi wa jinsi tofauti | Kumwondoa mwanafunzi bwenini bila kumrejeshea malipo ya pango. |
| 6 (e) | Kupika chakula bwenini pasipo kibali cha maandishi kutoka kwa Mshauri wa Wanafunzi au afisa ustawi wa jamii. | Kumwondoa mwanafunzi bwenini bila kumrejeshea malipo ya pango. |
| 6 (f) | Kuingilia au kuhamisha samani au vifaa vya aina yoyote kutoka bwenini bila ruhusa ya Mshauri wa Wanafunzi au afisa ustawi wa jamii. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi mitatu, na atatakiwa kulipa kwa uharibifu au upotevu wowote wa kifaa au samani hiyo. |
| 6 (g) | Kutumia baraza, dirisha au ukuta kwa ajili ya kuanika nguo au ufuaji wa aina yoyote. | Kutoa onyo kali. |
| 6 (h) | Kuingiza bwenini jokofu, mashine ya kukausha au kifaa chochote cha kupikia pasipo kibali cha maandishi kutoka kwa Mshauri wa Wanafunzi au afisa ustawi wa jamii. | Kumfukuza mwanafunzi bwenini bila kumrudishia malipo ya pango. |
| 6 (i) | Kuondoka bila kukabidhi vifaa vya malazi kwa afisa mwenye mamlaka. | Kutoa onyo kali na kumwagiza mwanafunzi kukabidhi vifaa vya malazi. |

*Tangazo la Serikali Na.149 (Linaendelea.)*

| KANUNI | KOSA LA NIDHAMU | ADHABU |
|---|---|---|
| 6 (j) | Kumzuia afisa wa Chuo au mtu yeyote aliyeidhinishwa kuingia chumbani kwa ajili ya ukarabati, ukaguzi au shughuli nyingine kama iliyoamuriwa. | Kumfukuza mwanafunzi bwenini bila kumrudishia malipo ya pango. |
| 6 (k) | Kutumia vifaa vya muziki na vyombo vingine vinavyotoa sauti bwenini na kusababisha usumbufu kwa wakazi wengine. | Kutoa onyo kali au kumfukuza mwanafunzi kwenye chumba bila kumrudishia malipo ya pango. |
| 6 (l) | Ulevi au uvutaji wa sigara bwenini | Kutoa onyo kali au kumfukuza mwanafunzi kutoka kwenye chumba bila kumrudishia malipo ya pango. |
| 6 (m) | Kuwakaribisha wageni wa jinsia tofauti bwenini baada ya saa nne usiku. | Kutoa onyo kali au kumfukuza mwanafunzi katika chumba bila kumrudishia malipo ya pango. |

ADHABU KWA MAKOSA YA KINIDHAMU YANAYOHUSIANA NA MGAHAWA NA JIKO

| KANUNI | KOSA LA NIDHAMU | ADHABU |
|---|---|---|
| 10(1) | Kuingia jikoni kwa mtoa huduma za mgahawa bila ruhusa ya mtoa huduma au Mshauri wa Wanafunzi au afisa ustawi wa jamii. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi mitatu. |
| 10(2) | Kuchukua chombo au kitu chochote kutoka mgahawani au eneo lolote ndani au nje ya Chuo bila kibali cha mtoa huduma, Mshauri wa Wanafunzi au afisa ustawi wa jamii. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi mitatu, na mwanafunzi atatakiwa kurudisha vyombo au vitu hivyo vikiwa na hali nzuri au kulipa fidia kwa uharibifu wowote.” |

Dar es Salaam,
20 Februari, 2025

KENNEDY M. HOSEA,
*Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi*